**PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

# MTIHANI WA KWANZA WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

# SOMO: MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI [06]

**TAREHE 09/03/2021** **MUDA: SAA 1:30**

**JINA LA MTAHINIWA:** ______________________________________________

**JINA LA SHULE:** ________________________________________________________

**WILAYA**: ____________________ **MKOA:** ____________________

## MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya majibu
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. Chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR)kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya (OMR)
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi
6. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa

<u>**SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA**</u>

**Chagua jibu sahihi kisha siliba herufi ya jibu hilo katika karatasi ya kujibia uliyopewa**

1. Vipi kati ya hivi vifuatavyo ni vyanzo vya moto wa asili?
   A. Uvutaji wa sigara na kulina asali
   B. Kuchoma misitu na kilimo
   C. Umeme wa radi na joto kali kutoka angani
   D. Shoti ya umeme na matumizi mabaya ya majiko ya gesi
   E. Mafuriko na milipuko ya volkeno
2. Miongoni mwa kanuni za uzimaji wa moto na uokoaji ni:
   A. Kugonga kengele au king'ora
   B. Kuwasha swichi za umeme
   C. Kufunga milango na kujificha chini ya meza
   D. Kukimbilia jengo linaloungua
   E. Kupiga simu kwa namba ya dharura 112
3. Mlima upi kati ya hii ifuatayo ni mfano wa volkano mfu?
   A. Oldonyo Lengai B. Kilimanjaro C. Meru D. Rungwe E. Usambara
4. Shughuli ipi ya binadamu kati ya hizi inaweza kusababisha kutokea kwaTsunami?
   A. Ukataji miti hovyo
   B. Moshi wa viwandani
   C. Ufugaji
   D. Kujaribu mabomu ya nyukilia katika bahari
   E. Kilimo kilichopitiliza
5. Mikoa ipi nchini Tanzania imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na janga la ukame?
   A. Kilimanjaro, Mwanza na Kagera
   B. Iringa, Mbeya na Ruvuma
   C. Dodoma, Singida na Shinyanga
   D. Tanga, Morogoro na Tabora
   E. Tanga, Mtwara na Njombe
6. Kuyeyuka kwa theluji katika mlima Kilimanjaro ni miongoni mwa athari za:
   A. Tetemeko la ardhi
   B. Milipuko ya volkano
   C. Kuongezeka kwa joto duniani
   D. Tsunami
   E. Mafuriko
7. Zifuatazo ni tahadhari za kuchukua ili kuepuka majanga ya moto, <u>**ISIPOKUWA:**</u>
   A. Kuchunguza vifaa vya umeme kabla ya kuvitumia
   B. Kuepuka kutumia vifaa vya umeme visivyo na ubora
   C. Kuepuka uvutaji wa sigari katika maeneo hatarishi kama vile sheli
   D. Kuielimisha jamii juu ya athari za moto
   E. Kuzuia matumizi ya majiko ya umeme na gesi
8. Kimiminika cha moto mithili ya uji mzito , kinachotokana na kuyeyuka kwa miamba kwa sababu ya joto kali hujulikana kama:
   A. Magma B. Lava C. Gamba D. Kiini E. Miamba geu
9. Miongoni mwa maendeleo makubwa ya katika historia ya mwanadamu katika kipindi cha zama za mawe za kati yalikuwa ni:
   A. Kutembea kwa miguu minne
   B. Kugunduliwa kwa chuma
   C. Ugunduzi wa moto
   D. Kuanzisha makazi ya kudumu
   E. Kilimo na ufugaji
10. Zama za maisha ya mwanadamu ambazo zimetawaliwa na utengezaji wa kompyuta pamoja na mashine mbali mbalimbali hujulikana kama:
    A. Homo habilisi
    B. Zama za mawe za mwisho
    C. Zama za mawe za kati
    D. Zama za mawe za mwisho
    E. Zama za Teknojia ya Kidijitali
11. Eneo la kihistoria ambalo ni maarufu kwa kuwepo mabaki ya mifumo ya kilimo cha umwagiliaji iliyokuwa inatumika hapo zamani ni:
    A. Engaruka B. Bonde la Olduvai C. Isimila D. Kaole E. Kondoa Irangi
12. Fuvu la kichwa cha mtu wa kale zaidi lililogunduliwa huko Olduvai Gorge na mwana akiolojia Daktari Luis Leakey pamoja na mkewe Mary Leakey mnamo mwaka 1959 lilipewa jina gani?
    A. Binadamu wa kisasa
    B. Homo erectus
    C. Homo habilis
    D. Zinjanthropus boisie
    E. Homo sapiens
13. Latitudo, mwinuko, sura ya nchi ,upepo pamoja na umbali kutoka baharini ni miongoni mwa vitu vinavyoathiri:
    A. Mfumo wa jua
    B. Tabia ya nchi
    C. Mkondo wa bahari
    D. Hali ya hewa
    E.Shughuli za binadamu
14. Mtu anayefanya kazi ya kurekodi na kutabiri hali ya hewa hujulikana kama:
    A. Mnadhimu
    B. Mnajimu
    C. Mtabiri wa hali ya hewa
    D. Mwanaanga
    E. Mwana antholopojia

15. Kuna umuhimu gani wa kujua hali ya hewa ya maeneo tunamoishi?
    A. Kupanga shughuli za kilimo
    B. Kuepuka mafuriko
    C. Kuepuka joto jingi
    D. Kuvuna maji ya mvua
    E. Kuzuia majanga ya asili
16. Matendo au tabia ambazo haziruhisiwa katika jamii kutokana na utamaduni wa jamii husika hujulikana kama:
    A. Taratibu B. Maadili C. Miiko D. Desturi E. Mila
17. Ushairi, riwaya na tamthiliya ni aina gani ya sanaa?
    A. Sanaa za vitendo B. Sanaa za maonyesho C. Sanaa za fasihi D. Sanaa ghibu E. Sanaa za michezo
18. Muingiliano kati ya jamii za Pwani ya Afrika Mashariki pamoja na Waroma na Wagiriki ulianza katika karne ipi?
    A. Karne ya 19 B. Karne ya 1 C. Karne ya 15 D. Karne ya 8 E. Karne ya 10
19. Nani aliyetawala Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mara baada ya kugawanywa kwa bara la Afrika katika mkutano wa Berlin?
    A. Cecil Rhodes wa Uingereza
    B. Karl Peters wa Ujerumani
    C. Mfalme Leopard wa Ubelgiji
    D. Jan van Riebeck Uholanzi
    E. Vasco da Gama wa Ureno
20. Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) iliundwa mwaka gani?
    A. 1967 B. 1995 C. 1982 D. 1992 E. 1990
21. Mwenyekiti wa kwanza wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) alikuwa nani?
    A. Filipe Yucinto Nyusi
    B. Kwame Nkurumah
    C. Haile Selassie
    D. Thabo Mbeki
    E. Cyril Ramaphosa
22. Ni bidhaa zipi kati ya hizi zifuatazo huweza kusafirishwa kwa njia ya bomba?
    A. Gesi, maji na mafuta
    B. Mafuta, hewa na magari
    C. Vimiminika, yabisi na gesi
    D. Mzao, madini na wanyama
    E. Watu, bidhaa na huduma
23. Nchi zipi kati ya hizi zifuatazo hufanya usafirishaji wa majini kupitia ziwa Nyasa?
    A. Tanzania, Zambia na Malawi
    B. Tanzania, Malawi Msumbiji
    C. Tanzania, Angola ana DRC
    D. Tanzania, Malawi na DRC
    E. Tanzania, Kenya na Malawi
24. Kwanini Zimbabwe, Afrika ya Kusini, Algeria na Kenya zilipata uhuru wao kwa njia yam tutu wa bunduki?
    A. Yalikuwa makoloni ya wareno
    B. Yalitawaliwa na wafaransa
    C. Yalikuwa makoloni ya walowezi
    D. Yalikuwa ni makoloni yaliyohifadhiwa
    E. Zilitawaliwa na Waingereza
25. Nchi zipi za Afrika zilipata uhuru wao kwa njia ya mapinduzi?
    A. Tanganyika na Zanzibar
    B. Rwanda na Burundi
    C. Somalia na Eritrea
    D. Liberia na Zanzibar
    E. Zanzibar na Misri
26. Mwalimu Julius K. Nyerere aliamua kustaafu nafasi ya Urais wa Tanzania kwa hiari yake mwenyewe mnamo mwaka gani?
    A. 1975 B. 1995 C. 1965 D. 1964 E. 1985
27. Shujaa wa Afrika aliyeongoza mapambano ya kudai uhuru na kufanikiwa kuikomboa Algeria kutoka mikononi mwa ukoloni mwa Wareno alikuwa nani?
    A. Nnamdi Benjamin Azikiwe
    B. Abubakar Tafawa Balewa
    C. Ahmed Ben Bella
    D. Augustino Neto
    E. Ahmed Sekou Toure
28. Ni tarehe ipi Dunia huwa katika umbali mrefu zaidi kutoka kwenye jua?
    A. 21 Machi B. 21 Juni C. 22 Desemba D. 3 Januari E. 4 Julai
29. Ni gimba lipi kati ya haya yafuatayo halibadili uelekeo wake wakati wa kupatwa kwa jua au kupatwa kwa mwezi?
    A. Jua B. Mwezi C. Dunia D. Zebaki E. Zohari
30. Ni aina gani ya kipimo cha ramani hutumika kuchora ramani za maeneo makubwa kama vile nchi, bara au ramani ya Dunia?
    A. Kipimio cha mstari
    B. Kipimio cha maneno
    C. Kipimio kidogo
    D. Kipimio cha kati
    E. Kipimio kikubwa
31. Ni maeneo gani ya Tanzania yana uoto wa asili wa mikoko?
    A. Katikati mwa Tanzania
    B. Kusini mwa Tanzania
    C. Mwambao wa Bahari ya Hindi
    D. Magharibi mwa Tanzania
    E.Kanda ya Ziwa

32. Kitendo cha kusafiri kutoka eneo moja hadi jingine kwa lengo la kustarehe, biashara, masomo au utafiri hujulikana kama:
A. Uchukuzi B. Ujasiriamali C. Usafirishaji D. Utalii E. Starehe
33. Ni kwa namna gani shughuli za utamaduni huchaingia kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla?
A. Kwa kutangaza utamaduni wa kigeni
B. Kwa kuhamasisha mila na desturi zisizofaa
C. Kwa kuwafundisha watu wawe wavivu
D. Kwa kupitia ukeketaji wa wanawake pamoja na jando na unyago
E. Kwa kuuza bidhaa za utamaduni kama vile vinyago na shanga
34. Nini madhara ya kuruhusu uingizwaji wa bidhaa za nje katika masoko ya ndani nchini Tanzania?
A. Kukua kwa pato la taifa C. Kukosa mitaji E. Ukuaji wa teknolojia
B. Kuanguka kwa viwanda vya ndani D. Kupungua kwa bidhaa za viwandani
35. Shughuli ipi ya uzalishaji mali kati ya hizi zifuatazo ina ajiri idadi kubwa ya watanzani?
A. Viwanda C. Ujasiriamali E. Kilimo
B. Utalii D. Uchimbaji wa madini
36. Mikoa ipi hapa Tanzania inaongoza kwa kilimo cha ndizi?
A. Kagera, Kilimanjaro na Mbeya C. Mbeya, Iringa na Njombe E. Dodoma, Singida na Tabora
B. Arusha, Kilimanjaro na Manyara D. Tanga, Kilimanjaro na Manyara
37. " Mjasiriamali lazima awe mbunifu". Nini maana ya ubunifu katika ujasiriamali?
A. Uwezo wa kukubali hasara D. Uwezo wa kufikiria na kubuni mbinu mpya
B. Kufanya kazi kwa bidii E. Uwezo wa kushawishi wengine
C. Kutokuwa na uwezo wa kufikiria njia mpya za kufanya mambo
38. Ni sehemu gani za mwili zinapaswa kufanyiwa usafi mara kwa mara wakati wa kubalehe?
A. Sodo na taulo C. Usoni na sehemu za siri E. Chupi na sodo
B. Macho na masikio D. Makwapani na sehemu za siri
39. Kwanini inashauriwa kuchemsha maji pamoja na majani ya chai wakati wa uandaaji wa chai ya maziwa?
A. Kupunguza gharama D. Kupunguza kiasi cha sukari kinachohitajika
B. Kuongeza ladha kwenye chai E. Kuifanya chai ichemke haraka
C. Kuifanya chai iwe nyeusi
40. Ni chombo kipi cha muziki kati ya hivi vifuatavyo hutoa sauti kwa kupigwa?
A. Filimbi C. Marimba E. Gitaa
B. Kinanda D. Zumari

## SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

**Jibu swali la 41-45 kwa kuandika majibu sahihi katika karatasi yako ya kujibia**

41. Mkutano wa Berlin ulikuwa na umuhimu gani kwa mataifa ya kibepari?
______________________________________________________________________

42. Kwanini inashauriwa kumwaga maji sakafuni kabla ya kuanza kupiga deki?
______________________________________________________________________

43. Binadamu wa kale alipataje chakula chake katika kipindi cha Zama za Mawe za Kale?
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

44. Sayari iliyo karibu zaidi na jua katika mfumo wa jua inaitwaje?
______________________________________________________________________

45. Waziri mkuu wa Tanzania aliyedumu madarakani kwa kipindi cha muda mrefu zaidi alikuwa nani?
______________________________________________________________________